Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 81 No. 225 | DH.HIJ-MUHAR 14423AH | AGOSTI 2021 | ZAHOOR 1400 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Hakika watu wanaomkurubia zaidi Ibrahimu ni wale waliomfuata yeye na Mtume huyu na walioamini; na Allah ndiye mlinzi wa waaminio. (Aali 'Imran 3:69)

اعجاز المسيح

MUUJIZA WA MASIHI MAU'UDI



Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] Masihi na Mahdi Aliyeahidiwa

Seyidna Ahmad[as] Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya alizaliwa katika kijiji cha Qadian. Hakuwahi kusoma shule wala madrasa yoyote, isipokuwa katika utoto wake alifundishwa kidogo nyumbani masomo ya awali na baadhi ya walimu. Baadhi ya masheikh walidhani kwamba mtu ambaye alizaliwa katika kijiji cha India na kutopata fursa ya kuenda kusoma madarasani huwa hawezi kujua lugha ya Kiarabu.

Hivyo, wakati Seyidna Ahmad[as] alipodai kuwa yeye ni Masihi Mau'udi na Imamu Mahdi, wapinzani wakapiga makelele

Endelea uk. 10



Makala uk 5

Maisha ya Mtume Mtukufu Muhammad[saw]

Yalivyosimuliwa na Hadhrat Mirza Bashir ud Din Mahmud Ahmad r.a. Khalifatul Masih wa pili wa Masihi Aliyeahidiwa[as]

Inaendelea Kutoka toleo lililopita

Vikwazo katika mahubiri baada ya vifo vya Hadhrat Khadija[ra] na Abu Twaalib na safari ya Taif ya Mtume[saw]



Sasa Muhammad[saw] na masahaba wake wakawa wameikosa athari ya Kinga ya Abu Twaalib na mwenzi wa nyumbani wa Mtume[saw], Hadhrat Khadija[ra], naye akawa hayuko naye tena. Kutokana na vifo vya wawili hao ikawa pia huruma ya watu kwake yeye na masahaba zake imepungua ambao kutokana na mahusiano yao, madhalimu walikuwa wakisita kufanya dhulma. Kutokana na majonzi ya kifo cha karibuni cha Abu Twaalib na kutokana na wasia wa Abu Twaalib, watu wachache waliokuwa maadui zake wakubwa pamwe na mdogo wa Abu Twaalib, Abu Lahab, wakamuunga mkono. Lakini watu wa Makka walipoichemsha jadhba yake kwa kusema hivi kuwa Muhammad[saw] anawafahamu wote wale wasioukubali umoja wa Mwenyezi Mungu kuwa ni wenye hatia na wenye kustahili adhabu, basi kutokana na ghera aliyokuwa nayo kwa mababu zake, akatengana nao na kuahidi kuwa sasa atafanya upinzani zaidi kuliko hapo awali.

Kwa kuwa watu waliishi miaka mitatu bila ya mawasiliano na ndugu na jamaa zao kulikosababishwa na maisha yale ya kutengwa, hivyo mahusiano yakawa sio ya nguvu. Watu wa Makka walikuwa wameshazoea kutoongea na Waislamu, hivyo uwanja wa mahubiri ukawa finyu.

Mtume[saw] alipoiona hali hii, basi akaamua kwamba aende kuwafikishia ujumbe wa Islam watu wa Taif badala ya wale wa Makka. Alikuwa bado akiyafikiria haya ambapo upinzani wa watu wa Makka ukaipa nguvu zaidi dhamira yake hii. Kwanza watu wa Makka walikuwa hawataki kusikiliza chochote. Pili wakawa wametumia njia hii kwamba wakawa hawamuachi Muhammad[saw] atembee huru mitaani. Alipokuwa akitoka nje wakawa wakimwagia udongo kichwani ili asiweze kukutana na watu. Siku moja alikuwa akirejea katika hali hii hii basi mmoja kati ya mabinti zake akawa akimpangusa udongo huku akilia. Akamwambia; Ewe binti yangu, usilie, kwa sababu kwa yakini kabisa Mungu Yu pamoja na baba yako.

Yeye[saw] alikuwa haogopi shida, lakini tatizo lilikuwa hivi kwamba watu hawakuwa tayari kusikiliza maneno yake. Kuhusiana na shida yeye alikuwa akiziona kuwa ni za lazima kutokea. Bali kwake siku iliyokuwa ya shida kuliko zote ilikuwa ni ile ambapo hakukuwa na yeyote wa kumsumbua. Imeandikwa kwamba siku moja Muhammad[saw] alitoka

Endelea uk. 3

Hala hala na picha za Khilafat uk. 11

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

MATEKA WA HISTORIA

Mjadala wa kusisimua na kurutubisha fikra unaendelea miongoni mwa wanamajumui na wapenzi wa Mama Afrika. Suala lisilowapa usingizi ni kwa nini bara hili liliolozungukwa na bahari, mito, lenye madini yote yanayotafutwa hii leo kwa udi na uvumba, ardhi nzuri na yenye rutuba utadhani imepakwa mafuta, vivutio kwa watalii, kwa nini, lakini kwa nini, bara hili halionyeshi dalili hata moja ya kusonga mbele ila kila uchao linazidi kudidimia na leo yake inakuwa mbaya zaidi kuliko jana yake?

Kinachowaumiza na kuweka ganzi katika nyoyo zao ni kuwa bara la Asia ambalo limepitia madhila kama ilivyopitia Afrika yaani kutawaliwa, lakini Asia hivi leo inasonga mbele na kishindo chake kinasikika kwa wale waliojivika sare za kuwa polisi wa dunia. Zipi sababu zinazotolewa za kueleza kwa nini Afrika imezama katika tope. Moja ya sababu ambayo imeshika kasi ni ile iliyofafanuliwa na mwanaharakati na mwanahistoria marufu, Walter Rodney katika Kitabu chake – *How Europe Underdeveloped Africa.* Afrika ilivyovamiwa ukaendeshwa utumwa, uliovunja miundo mbinu na taasisi zilizokuwepo. Ikajengeka hofu. Mgawanyiko. Kutoaminiana. Bara la Afrika likapoteza nguvu kazi. Kana kwamba hiyo haitoshi ukaingia ukoloni. Kwa mabavu wakaingia. Na kwa mabavu wakatawala. Ardhi wakachukua. Kazi za kulazimishwa tena kwa malipo hafifu. Kwa mfumo wa elimu waliouanzisha tukajengewa kutojiamini. Kudharau kila kitu chetu. Vikabomolewa viwanda vyetu. Dawa zetu zikapewa jina hovyo. Tukalazimishwa kulima tusichokula na kula tusicholima. Kila tulichokifanya ni kutimiza mahitaji yao sio yetu. Mradi huo ulipokwisha ukaingia mrado wa ukoloni mambo leo. Watawala wako London, Washington, Brussels, Paris na huku wanaotekeleza matakwa yao ni wale ambao Chachage anawaita Makuadi wa Soko huria. Hapana shaka yoyote ni jambo la lazima kuifahamu historia yetu, ni muhimu kufahamu tulikotoka na kwa vipi tumefika tulipo kwa hivi sasa. Hatuwezi kupuuza yaliyopita jana.

Jambo la msingi linalotukabili kwa hivi sasa, mpaka lini na kwa kiasi gani tutaendelea kuwa mateka na historia yetu? Lini historia yetu itakuwa kichocheo na kututia uchungu ili tuweze kuendelea? Lini tutaacha kutumia kisingizio cha historia katika kuhalalisha haya tunayoyafanya hivi leo? Rushwa iliyoota kama uyoga katika Afrika, viongozi walioweka pamba masikioni mwao, wakishiriki katika mikataba ya kutudhuru. Kwa nini hatuwezi kuitumia historia baada ya historia kututumia sisi? Wamefanya hivyo wale wengine na mfano mzuri ni Asia.

Lakini tukumbuke jambo ambalo tunakumbushwa na mhusika katika riwaya maarufu ya Peta Abrahams *A Wreath for Udomo*. Mhusika huyo anasikitika "Ndugu zetu Waafrika wanakosa mguso na mtiririko wa historia. Wanadhani wao peke yao ndio wametawaliwa. Kutawaliwa na dhana kongwe." Ni kweli historia inathibitisha hilo, Uingereza iliwahi kutawaliwa na Roma, Marekani iliwahi kutawaliwa na Uingereza. Nchi za Asia zimetawaliwa. Kilichofanyika, wamepepeta na kutenganisha mchele na pumba. Mchele wamechukua na pumba wamewaachia wenyewe. Sisi katika Afrika tumechukua pumba na mchele tumewaachia. Mpaka wa leo hata majina yaliyolazimishwa kwetu bado yanatumika. Hilo nalo linahitaji rasilimali? Unaendeleaje kuliita ziwa Lweru, Victoria? Si mikogo hiyo mtu anapomwaga kimombo, Kifaransa na kichekesho anapozungumza lugha za Afrika?

Ni miaka 60 na ushehe toka wakoloni waondoke. Hatuwezi kujilisha. Kumbuka Ethiopia watoto wanaendelea kukaa chini, bei ya umeme inaongezeka kila siku. Bara limezungukwa mito lakini watu hawana maji ya kunywa. Hospitali gharama za matibabu zinatisha. Miradi minene iliyojaa ufisadi inaendelea kutapakaa katika Afrika. Chaguzi zikitokea sehemu hiyo inageuka jahanamu, mwaka mzima wote huo maofisini, nyumbani, mazungumzo, ni juu ya uchaguzi.

Ni rahisi, tena rahisi sana kuonyesha upungufu. Kuonyesha udhaifu. Swali la msingi ambalo aliwahi kuuliza V.I. Lenin kiongozi wa mapinduzi ya Urusi, nini kifanyike? Tunashauri yafuatayo;

Uongozi

Laana ya Afrika kama kweli inaweza kuitwa laana imetokana na viongozi. Sio wote bali wengine wametusaliti kama anavyotuonyesha Ayi kwei Amah kwenye riwaya yake *The Beautiful Ones Are Not Yet Born*. Uchu wa mali umewapumbaza na kufanya mambo ya aibu. Kusisitiza kuwa mtu hawezi kunywa maji ya hapa Afrika hadi yatoke Paris! Nguo zipigwe pasi London. Watibiwe ughaibuni, magari ya kifahari, wengine wamelewa hadi kusema mimi ndio taifa. Afrika inahitaji viongozi wanaomcha Allah. Waelewe kuwa wataulizwa juu ya hawa waliopewa kuongoza. Wanyenyekevu wanaoelewa kwamba wao ni watumishi na sio mabwana.

Huwezi kuongoza peke yako. Hata kama u mwema kiasi gani huwezi kudumu milele. Kinachotakiwa ni ujengaji wa taasisi imara. Taasisi zinazojitambua na sio kuwajibika tu kwa Rais bali kwa umma. Taasisi huru zinazoweza kusimamia maslahi ya umma. Taasisi ambazo kiongozi akipiga filimbi taasisi zote zinacheza haziwezi kusaidia sana maendeleo ya nchi.

Ukombozi wa fikra, uzalendo, mahaba ya nchi, ghera, vyote hivyo vinatokana na mfumo wa elimu yetu. **Elimu** tuliyonayo ni makombo tuliyoachiwa na wakoloni. Na mla makombo hatononoki. Tunataka mfumo wa elimu unaangazia uhalisia wa Afrika, matarajio na matumaini ya Afrika. Tutoe kipaumbele kwa elimu. Shule iwe shule. Waalimu wapewe hadhi yao. Marupurupu yazingatiwe. Unawezaje kucheza na hawa wanaotengeneza Afrika inayotakiwa kupaa kama tai?

Elimu yetu ikiimarika tutapata wataalamu ambao sifa yako kubwa ni uzalendo na elimu. Kazi zitatolewa si kwa sifa ya mtoto wa shangazi, binamu bali kwa kuwa na sifa. Sifa zitakuwa kigezo cha kupewa majukumu.

Mapinduzi ya viwanda yanayokwenda sambamba na kilimo yatatujenga kujitegemea ambayo ndio hasa alama ya uhuru. Hii itawezekana kama tuna umeme wa kuaminika na rahisi. Ni kichekesho kufikiria juu ya mapenzi ya viwanda kama una umeme unaozima mithili ya koroboi.

Tukubali mauwa ya fikra yachanue. Wasiwepo wale wanaodhani wana hati miliki ya ukweli wote au wao ni wazalendo zaidi kuliko wengine. Sote tuna uchungu na Afrika, na hivyo sote tushindane katika kuitendea yaliyo mema Mama Afrika. Mungu Ibariki Afrika.

Jamia Ahmadiyya Washiriki Jalsa Salana Uingereza 2021 Mubashara



Na **Sheikh Abid Butt**
Jamia, Morogoro

Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu mwaka huu wa 2021 wanajumuiya nchini Uingereza walifanya Jalsa Salana iliyochukua taswira ya kimataifa kutokana na uwepo wa Hadhrat Huzoor Aqdas (a.t.ba).

Itakumbukwa kuwa kwa miaka kadhaa sasa Jalsa Salana zimekuwa hazifanyiki hapa nchini na hata ile ya kimataifa ya Uingereza. Hii ni kutokana na Janga la virusi vya Korona kusambaa duniani.

Lakini mwaka huu kwa msaada wa Allah katika nchi ya Uingereza angalau imeruhusiwa kufanya Jalsa bila ya wahudhuriaji kutoka nje ya Uingereza. Wanajumuiya katika nchi mbalimbali duniani walifuatilia mkutano huu kupitia idhaa yetu ya MTA. Hapa nchini mpango maalum ulifanyika katika chuo chetu cha Jamia Ahmadiyya ili kushiriki moja kwa moja katika jalsa hiyo kwa njia ya intaneti. Wanafunzi, Wakufunzi na hata wanajumuiya wengine pia walishiriki huku wakiwa wanaonana mubashara. Ikumbukwe kuwa Jamia Ahmadiyya kilikuwa ni kituo pekee nchini kuonyesha Jalsa hii ya Uingereza kwa mpango huu maalum. Washiriki walihudhuria na kushiriki katika programu zote, kuanzia tukio la kwanza la upandishaji wa bendera na kufuatiwa na hotuba ya Huzur Aqdas {a.t.b.a.} lililofanyika siku ya Ijumaa tarehe 6/08/2021 saa 12: 15 jioni hadi tukio la mwisho ambalo ni hotuba ya kufunga mkutano iliyotolewa na Amiirul-muminiin Hadhrat Khalifatul-masihil-khaamis {a.t.b.a} siku ya Jumapili ya tarehe 8/8/2021 kuanzia saa 1:15 hadi saa 2:40 usiku. Alhamdulillah.

Aidha taarifa zilizopokelewa kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini, wanajumuiya wanashukurunakupongeza mno mpango huu ambao umewaunganisha moja kwa moja na Khalifa wa zama.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi:	Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri:	Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta:	Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji:	Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji:	Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:	1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga 2. Mahmood Hamsin Mubiru. 3. Jamil Mwanga. 4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Maisha ya Mtume Muhammad *saw*



Kutoka uk. 1

nje kwenda kuhubiri mitaani lakini siku hiyo, sawa na hila iliyopangwa, hakuna mtu yeyote, si mtumwa si muungwana, aliyeongea naye na wala hawakumpa usumbufu wa aina yoyote ule. Hapo Mtume*saw* akawa amelala akiwa kimya aliyejawa na uchungu na huzuni, kiasi ya kwamba Mwenyezi Mungu Akamfariji na kumwambia: Nenda tena na tena kwa watu uwatahadharishe na wala usijali kupuuza kwao.

Hivyo Mtume*saw* alikuwa hahangaishwi na jambo hili kwamba watu walikuwa wakimsumbua. Lakini Nabii wa Mwenyezi Mungu aliyeinuliwa kwa ajili ya kuiongoza dunia angewezaje kulivumilia jambo hili kwamba watu wasiseme naye na wasiwe tayari kulisikiliza neno lake. Maisha yasiyokuwa na faida ya aina hii ndio ulikuwa usumbufu mkubwa kuliko wote kwa ajili yake.

Hivyo akachukua uamuzi usiotetereka kwamba sasa ataelekea huko Taif na kuwafikishia watu wa Taif ujumbe wa Mwenyezi Mungu. Na hivi ndivyo ilivyokadiriwa kwa manabii wa Mwenyezi Mungu kwamba watoke hapa na kwenda kule wakiwahubiria watu wa kaumu mbali mbali. Yalitokea hivi hivi kwa nabii Musa a.s. Wakati mwingine aliwahutubia watu wa Firauni, wakati mwingine wana wa Is haq na wakati mwingine watu wa Midiani. Hata Hadhrat Isa a.s. pia wakati mwingine shauku yake ya Mahubiri ilimlazimisha kuwahutubia watu wa Galileya, wakati mwingine watu wa mlima Jordan, wakati mwingine watu wa Yerusalem na wakati mwingine watu wengine.

Watu wa Makka walipokataa kuyasikiliza maneno yake na kuchukua uamuzi huu kwamba apigwe na kunyukwa na asisikilizwe asilan, basi akaamua kuelekea upande wa Taif. Taif ni mji uliopo takriban maili sitini hivi upande wa Kusini Mashariki wa Makka, mji uliokuwa mashuhuri kwa matunda yake na mazao yake. Watu wa mji huu hawakupitwa na watu wa Makka katika kuabudu masanamu. Mbali na masanamu yaliyowekwa ndani ya Kaaba, kulikuwepo na sanamu moja mashuhuri lililoitwa Laat lililokuwa likitoa umuhimu wa Taif ambapo Waarabu walikuwa wakitoka sehemu za mbali kwa ajili ya kulizuru.

Watu wa Taif walikuwa na mahusiano sana ya kindugu na watu wa Makka na kati ya Taif na Makka kulikuwa na mashamba mengi yenye rutuba yaliyokuwa yakimilikiwa na watu wa Makka. Mtume*saw* alipowasili Taif, basi viongozi wa huko wakaanza kuja kukutana naye, lakini hakukuwa na mtu yeyote aliyekuwa tayari kuikubali haki. Watu wa kawaida nao wakawafuata viongozi wao na wakautazama ujumbe wa Mwenyezi Mungu kwa mtazamo wa chuki. Kwa mtazamo wa watu wa dunia, Nabii asiyekuwa na kitu wala msaidizi huwa anakuwa tu ni mtu wa kuchukiwa; Wao wanajua tu kuisikiliza sauti ya silaha na ya majeshi.

Habari zilikuwa tayari zimeshawasili kuhusiana naye. Alipowasili Taif na wao kumuona kuwa, badala ya kuwa pamoja na jeshi na Jath (comp. page 133 line 6 top), yeye alikuwa tu ameandamana na Zaid akiyazungukia maeneo mashuhuri ya Taif akifanya mahubiri, basi wale waliokuwa vipofu wa moyo wakawa hawakumuona aliyekuwa mbele yao kuwa ni nabii wa Mwenyezi Mungu, bali walimuona tu kuwa ni mtu wa kuchukiza na wa kustahili kuburuzwa na wakadhani kwamba huenda kumfikishia huyo shida na usumbufu kutatufanya tuonekane kuwa ni watu wenye kuheshimika mbele ya viongozi wa kaumu.

Siku moja walijumuika wakiwa pamoja na mbwa. Wakawahamasisha vijana na kujaza mawe ndani ya mifuko yao na wakaanza, bila huruma, kumshambulia Mtume*saw* kwa mawe. Wakamfukuza Mtume*saw* hadi nje ya mji. Miguu yake ikawa inavuja damu na Zaid akawa ameumia sana kutokana na kumuokoa Mtume*saw* lakini hata hivyo mioyo ya madhalimu hao ikawa bado haijapoa. Wakaendelea tu kuwaandama hadi maili nyingi nje ya mji kwenye maeneo ya milimani.

Wakati watu hawa walipokuwa wakiwafukuza, alitazama mbinguni, akihofia isije watu hawa wakateremkiwa na ghadhabu ya Mwenyezi Mungu, na kuomba kwa uchungu na unyenyekevu sana akisema: Ewe Muabudiwa! Wasamehe watu hawa, kwani hawajui wanalolifanya.

Akiwa amejeruhiwa na kuchoka, akiwa amefukuzwa na watu wa dunia, akjihifadhi chini ya kivuli cha mzabibu ndani ya shamba la mizabibu. Shamba hili la mizabibu lilikuwa linamilikiwa na viongozi wawili wa huko Makka. Kiongozi yule aliyekuwemo ndani ya shamba hilo la mizabibu kwa wakati huo alikuwa ni adui mkubwa na wa siku nyingi aliyepitisha, hapo awali, miaka kumi ya maisha yake katika upinzani (dhidi ya Mtume*saw*).

Yawezekana wakati huo hisia zake zilivutwa na jambo hili kwamba watu wa Taif walikuwa wamemjeruhi mtu wa Makka, au wakati huo ulikuwa ndio ule wakati ambapo mbegu ya wema ilikuwa ikichipua ndani ya mioyo yao. Alimpatia mtumwa wake aliyeitwa Addaas sinia lililokuwa limejaa zabibu na kumwambia: Nenda kawapatie wale wasafiri. Huyu Addaas alikuwa ni Mkristo aliyetokea Ninenwa.

Alipomkabidhi zabibu zile Mtume wa Mungu, Muhammad*saw* naye akazipokea zabibu zile huku akisema: Nazipokea kwa jina la Allah Aliye mwingi wa Rehema, mwingi wa Ukarimu. Hapo moyo wake (Addaas) ukaukumbuka Ukristo. Akahisi kwamba mbele yake alikuwa ameketi nabii fulani wa Mwenyezi Mungu aliyekuwa akiongea lugha kama ya manabii wa Kiisraeli. Mtume*saw* akamuuliza: "Wewe u mwenyeji wa wapi?" Alipomjibu kuwa ni wa Ninenwa, basi Mtume*saw* akamwambia: "Yule mtu mwema Yunus aliyekuwa mwana wa Matta, na aliyekuwa mwenyeji wa Ninenwa, alikuwa ni nabii wa Mwenyezi Mungu kama mimi." Kisha akaanza kumhubiria dini yake. Kufumba na kufumbua mshangao wa Addaas ukageukia katika kustaajabu na kuvutiwa. Kustaajabu kukabadilikia kwenye imani na ndani ya muda mfupi tu, mtumwa yule aliyekuwa mgeni kabisa, alimkumbatia Mtume Muhammad*saw* huku macho yake yakiwa yanatiririka machozi na kuanza kumbusu kichwa chake, mikono yake na miguu yake.

Baada ya kumaliza maongezi yake na Addaas, Mtume*saw* alimuelekea Mwenyezi Mungu na kuomba dua hii:

"Ee Mola wangu! ninakushatakia juu ya madhaifu yangu, upungufu wangu wa nyenzo na kuonekana kwangu duni machoni mwa watu, lakini Wewe ni Mungu wa walio masikini na walio dhaifu na Wewe ni Mungu wangu pia. Utaniacha mikononi mwa nani? Je utanitelekeza mikononi mwa wageni wanaoniburuza huku na kule? au mikononi mwa adui yule aliyenishinda nyumbani kwangu? Kama hujanikasirikia basi mimi siwajali chochote hao maadui. Huruma yako iwe pamoja nami na 'Aafiyat yako ipanuke zaidi kwa ajili yangu. Ninataka kimbilio kwenye nuru ya Uso Wako. Ni kazi Yako Wewe tu kulifukuza giza duniani na kuleta amani humu duniani na Akhera. Isiniangukie hasira na ghera Yako. Hata kama Unakasirika basi ni kwa sababu hii tu ya kuidhihirisha tena furaha Yako na mbali nawe hakuna sehemu yoyote yenye nguvu ya uhakika na kimbilio la kweli.

Baada ya kuomba dua hii akaelekea Makka, lakini akakaa kwa muda (kabla ya kuingia Makka) sehemu fulani iliyoitwa Nakhla. Alipumzika hapo kwa siku chache na kisha kuelekea Makka. Lakini sawa na desturi ya Waarabu, kutokana na hali ya vita, alikuwa si raia tena wa Makka baada ya kuondoka Makka. Sasa watu wa Makka wakawa na hiari ya kumruhusu aje au kutomruhusu. Ndio sababu akamtumia ujumbe kiongozi fulani wa Makka, Mut'am bin Addiy, akimwambia: Mimi nataka kuingia Makka, je, sawa na desturi ya Waarabu, waniruhusu kuingia? Mut'am alikuwa ni mtu mwenye asili ya wema ingawa alikuwa ni adui mkubwa. Wakati huo huo akawakusanya watoto wake na ndugu zake na kuelekea kwenye uwanja wa Kaaba wakiwa na silaha na kumtumia ujumbe kwamba anampa ruhusa ya kuingia Makka. Mtume*saw* akaingia Makka na kuizunguka Kaaba na Mu'tam pamwe na wanawe na ndugu na jamaa zake wakamsindikiza hadi nyumbani wakiwa na silaha zao mikononi. Hiyo haikuwa hifadhi, kwa sababu baada ya hapo dhulma zikaendelea dhidi ya Mtume*saw* na Mut'am hakutoa hifadhi yoyote kwake, bali ile ilikuwa ni ruhusa tu ya kidesturi ya kuingilia Makka.

Kuhusiana na safari yake hii, hata maadui nao walikiri kuwa katika safari yake hii ya Taif alionyesha mfano wa kujitolea na uvumilivu usio na kifani. Sir William Muir ameandika hivi ndani ya kitabu chake kiitwacho Muhammad kwamba:

"Kuna hali fulani ya kusifika na ya kishujaa katika safari hii ya Muhammad ya huko Taif. Akiwa mpweke, aliyedharauliwa na kukataliwa na watu wake, akisonga mbele kwa ujasiri kwa jina la Mwenyezi Mungu, kama Yona wa Ninenwa, na kuuita mji wa kipagani akiutaka utubu na ku uunga mkono ujumbe wake. inatoa mwanga wenye nguvu wa kiwango kikubwa cha imani aliyokuwa nayo ya kuwa ujumbe wake umetoka kwa Mwenyezi Mungu.

Makka ikafungua tena milango yake ya maudhi na kejeli. Mji wa Nabii wa Mwenyezi Mungu ukaanza tena kuwa mfano wa Jahannam kwa ajili yake. Lakini juu ya hayo, Muhammad*saw* akaendelea, kwa ujasiri, kuwafikishia watu ujumbe wa Mwenyezi Mungu. Sauti za Mungu ni Mmoja, Mungu ni Mmoja zikaanza kupaa kwenye mitaa na vichochoro vya Makka. Akaanza kuwatolea, kwa huba, upendo na nia njema, mawaidha dhidi ya ibada ya masanamu. Watu walikuwa wakikimbia naye akawa akiwafuata nyuma. Watu walikuwa wakimgeuzia uso upande lakini bado tu aliendelea kuwafikishia ujumbe. Taratibu ukweli ukaanza kushamiri. Wale Waislamu wachache waliobakia Makka kwa kutohamia Uhabeshi, wao ndani kwa ndani walikuwa wakiwahubiria ndugu na jamaa zao, majirani zao, marafiki zao na wenzao. Mioyo ya baadhi yao ilikuwa ikipata nuru ya imani na wakawa wakijidhihirisha kwa kutangaza dini yao na wakawa wakishiriki na ndugu zao katika kupata vipigo na masumbufu.

Lakini ni wachache mno walioiona na nuru na halafu kutopata uwezo wa kutoikubali. Wao walikuwa wakiisubiri siku ile ambapo ufalme wa Mwenyezi Mungu utakapokuja duniani nao wapate kuingia humo.

Itaendelea toleo Lijalo

Baraka za Jalsa Zilizoshuhudiwa Ulimwenguni Kote

Kutoka uk. 12

Nigeria n.k.w. Kwa ujumla ni maeneo 37 katika nchi 22 yaliyopata nafasi kushiriki katika Jalsa Salana Mubashara.

Maoni Ya Watu Waliotazama Jalsa Salana ya Uingereza:

Mgeni wa Nijer anasema; baada ya kuona Jalsa akafikiria kuwa laiti kama waislamu wengine wangekua kama hawa Waahmadiyya, basi waislamu hao wangekuwa na umoja usio na mfano.

Zambia: Katika tawi fulani walikuwepo wageni 35. Kutoka miongoni mwao mwalimu mmoja Mkristo alisema kuwa Dini ya Uislamu ni Dini ya Ukweli nimejifunza mengi katika Jalsa Salana.

Gabon: Afisa wa polisi alisikia tukiola kujiunga la mwanajumuiya mmoja wa Lebanoni, akaomba aone MTA mwenyewe. Hapo akapewa nafasi ya kufungua mtandao wa Youtube na kufungua idhaa ya MTA Fransa ili aweze kuona mwenyewe vikao vyote.

Nigeria: Mgeni mmoja baada ya kusikiliza hotuba mbali mbali za Jalsa akasema huenda nitajiunga na jumuiya hivi karibuni. Mgeni mwingine anasema ameathirika sana na hotuba za Hadhrat Khalifatul Masih (atba).

Japani: Mgeni Bw. Osamu Sahib aliona Jalsa na akasikia hotuba ya Agosti tarehe 6. Yeye anasema amekumbuka ihsani ya jumuiya kwamba mnamo tarehe 10 ya mwezi huu wa Agosti mwaka 1945 wakati bomu la atomiki lilipotupwa juu ya Heroshima na maelfu ya watu wakaangamizwa, wakati huo Hadhrat Khalifatul Masih wa Pili (r.a.) alipaza sauti dhidi ya dhulma hiyo. Mgeni huyu alipendekeza kuwa ingefaa iwepo idhaa ya MTA Japani kama ilivyowekwa MTA Afrika.

Lusaka Zambia: Mgeni mwingine alisema kwamba tumejifunza jambo moja kuwa Ulislamu unahubiri usawa wa wanawake. Dini ya Uislamu ni dini ya pekee inayolinda haki za wanawake. Inaruhusu kuoa zaidi ya mara moja lakini kwa masharti ya uadilifu.

Nijer Kasau: Mgeni Mhandisi mmoja alisema jumuiya ina nidhamu nzuri sana. Mgeni mwingine wa kike alisifu sana mafundisho ya Dini Tukufu ya Kiislam yanayohusu haki za wanawake na akasema kuwa kama mahubiri yao yanafanana na vitendo vyao basi wao ni watu wa mfano.

Khalifa Mtukufu (atba) anasema: inafaa zaidi tupate funzo kutokana na kauli hiyo. Khalifa Mtukufu (aba) anasema: kwa ujumla huu ni ujumbe kwa wanaume wote waboreshe khulka zao wasijidanganye kuwa wao ni bora.



Washiriki wa Jalsa Salana ya Uingereza 2021 wakisikiliza hotuba ya ufungaji iliyotolewa na Khalifatul Masih V[atba]

Mgeni mwingine alialikwa kwenye Jalsa Salana naye akakubali mwaliko huu akidhania kuwa mkutano huu utakuwa kama maonesho fulani ya kawaida ya kidunia lakini baada ya kuona vikao vya Jalsa Salana alivipenda sana mpaka akabaki siku zote 3.

Guinea Konakri: Wakati wa Kikao cha Jalsa Salana umeme ukakatika na kawaida ni kuwa unapokatika huchukua muda mrefu kurejea. Ndipo Wanajumuiya walipomwomba Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu Akaurudisha kabla ya Khalifa Mtukufu (atba) hajasimama kutoa Hotuba yake na mara tu baada ya hotuba ya Hazrat Khalifatul Masih (atba) kwisha umeme ukakatika tena.

Cameroon: Chifu mmoja asiyekuwa Mwahmadiyya anasema tumesikia huko nyuma kuwa Masihi atakapofika ataonekana kwa watu wote. Kauli hii imetimia leo kwa kuiona Jalsa Salana.

Tanzania: Bibie mmoja anasema; mimi sijawahi kuona kongamano lolote la aina hii lisilokuwa na mambo ya kidunia ndani yake.

Zambia Losangazi: Bwana Ali ni kiongozi wa eneo lake aliyejiunga na jumuiya mwaka 2021. Alipojiunga yeye na watu wake wakatembelewa na masheikh wasiokuwa waahmadiyya na walihubiriwa dhidi ya Jamaat. Lakini kwa kushiriki katika Jalsa Salana akajua hakika haswa ya Jamaat.

Mgeni mmoja kutoka Malaysia anasema; alikuwa hajawahi kwenda Uingereza lakini kwa kuhudhuria Jalsa Salana kupitia mitandao amepata baraka zote.

Brazili: Mgeni mmoja anasema nimepata bahati nzuri ya kushiriki na kusikiliza vikao hivi na kujiunga na Jumuiya hii.



Waahmadiyya wa Uholanzi wakitazama Jalsa Salana ya Uingereza kupitia MTA katika moja misikiti nchini humo.

Guinea Bissau: watu walisafiri kwa miguu kilomita 8 kuja kusikiliza Jalsa Salana.

Guyana: Mshiriki mwingine baada ya kutazama Jalsa Salana ansema; mimi nimepata uzoefu wa kipekee na alisifu usomaji wa Kurani tukufu uliofanywa na Lajna. Naye akavutiwa sana na huduma za wafanyakazi wa kujitolea, na hotuba za Khalifa Mtukufu (atba).

Austria: Mwanamke mwahmadiya anasema; nilitokwa na machozi niliposikia hotuba zote za Hadhrat Khalifatul Masih V (atba).

Waliojiunga wakati wa Jalsa Salana Uingereza:

Mtu mmoja kutoka Ivory Coast amejiunga baada ya kusikia Hotuba za Hadhrat Khalifatul Masih V (atba).

Watu 12 kutoka eneo la Gamboma Kongo wamejuinga na Jamaat kwa sababu ya kutazama Jalsa Salana.

Katika sehemu nyingine watu walifika baada ya kusafiri kilometa 18 na wengine kilometa 30, mwishowe watu 127 wakajiunga na Jumuiya.

Ndugu fulani kwa kuona vipindi vya Jalsa Salana akaathirika sana na baada ya kuongea na familia yake, wote wakajiunga na Jamaat.

Baadhi ya Watu kutoka Guinie Bisau walisikiliza vipindi vya Jalsa Salana na baadae wakasema; jumuiya hii ni ya pekee yenye Imamu. Nayo ndiyo ile tuliyokuwa tunaitafuta, nao wakajiunga.

Baadhi ya watu kutoka Kongo Brazaville, Niger, na Cameroon wamejiunga na Jumuiya baada ya kusikiliza na kuathirika na Hotuba ya Khalifa Mtukufu (atba).

Katika nchi ya Mali watu wamejiunga na Jumuiya baada ya kusikiliza vipindi vya Jalsa Salana kwa njia ya Redio za Jumuiya.

Ndugu mmoja wa eneo fulani baada ya kusikiliza Hotuba za Hazrat Khalifatul Masih (atba) na vipindi vingine vya Jalsa akasema; sisi tumejiunga nasi tutatoa michango pia. Katika Mkoa wa Kai watu waliuliza masharti ya kujiunga na Jumuiya nao baada ya Jalsa wakajiunga.

Nchini Ghana katika jimbo la Acra watu waliokusanyika kusikiliza vipindi vya Jalsa ni 2,500. Mjini Komasi wametazama watu 2000. Katika jimbo la Upper West, eneo la Wah watu 2,000 wamekusanyika katika sehemu 12 kwa ajili ya kutazama wakati wa mkutano wa Jalsa Salana UK.

Bw. Akram Sahib Kehlani kutoka Yemeni anasema: Leo

Inaendelea uk. 5

Baraka za Jalsa Zilizoshuhudiwa Ulimwenguni Kote

Kutoka uk. 4

tumefufuliwa na Imamu wetu (atba) na tumepata mwongozo na mwelekeo mzuri na kama tukifuata maagizo haya yaliyotolewa na Khalifa Mtukufu (aba) tutaongoka dunia nzima.

Bw. Hamid Sahib kutoka nchi ya Jordan anasema: Watu wameshiriki katika Jalsa Salana ya mwaka huu kutoka katika sehemu zote za dunia nzima kwa kupitia MTA. Na mimi ninafananisha mandhari haya na mandhari ya matunda ya Peponi.

Bw. Muhammad Sham Sahib kutoka nchi ya Syria anasema: Waislamu Waahmadiyya wamekusanyika chini ya bendera ya Jumuiya nayo ni sawa na maelezo ya Aya hii ya Qurani Tukufu: "Na Mwenyezi Mungu Ameiunganisha mioyo yao; hata kama ungalitoa yote yaliyomo ardhini usingaliweza kuiunga mioyo yao, lakini Mwenyezi Mungu ndiye Aliyewaunganisha." (Surah Al Anfaal 8:64)

Sisi sote tumekumbushwa kuleta mageuzi ya kiroho miongoni mwetu.

Mwanajumuiya mmoja kutoka West Bank Palestine anasema; inafaa tulete mageuzi ya kiroho katika khulka na vitendo vyetu. Dunia ya Kiahmadiyya iko chini ya uongozi wa Khalifatul Masih (aba).

Ndugu mwingine kutoka Niger alifurahi sana baada ya kusikiliza Jalsa Salana katika lugha ya Kihausa, lugha hii inazungumzwa na watu Millioni 50 Afrika.

Nchini Australia watu wamefuatilia vipindi vya Jalsa pamoja na tofauti kubwa ya majira iliyopo baina ya nchi yao na UK.

Mbali na hayo watu wengi kutoka nchi za Brazil, Kirgizistan, Guetemala, Luithuinia walisimulia hisia zao baada ya kuona Jalsa Salana.

Ufikishaji Ujumbe wa Jumuiya kwa Watawala Na Vyombo Vya Habari:

Jumbe za viongozi wa Serikali na watawala 109 kutoka Mataifa 9 zimetumwa ili zisomwe katika Jalsa Salana Uingereza. Ukiwemo ujumbe wa Raisi wa Uingereza, Kiongozi wa Chama Cha Labor Uingereza, Kiongozi wa Chama cha Leb Dem, Mawaziri 8, Manaibu Mawaziri 4 na Mamea 13.

MTA Afrika na vipindi vya Jalsa Salana UK vimeoneshwa katika mataifa 14 ya Afrika.

Tafsiri ya Kihausa imefanywa mara ya kwanza.

Watu Milioni 60 wameona taarifa za Jalsa Salana. Katika nchi ya Uganda wapinzani wa Jumuiya walifanya propaganda kabla ya Jalsa Salana lakini propaganda hiyo imeleta watu wengi ili kusikiliza Jalsa Salana na wakapendezwa na mafundisho ya Jumuiya.

Padre Mkatoliki wa Uganda alisikia Hotuba ya Khalifa Mtukufu (atba) aliyoitoa kwa Lajna na mafundisho haya yalimpendeza sana. Ndipo alipoomba mswada wa hotuba hiyo, utakaotumwa kwake insha'Allah.

Rafiki mwingine kutoka Liberia asiyekuwa Mwahmadiyya alipoona Aya ya Qurani Tukufu ya Khaatamun Nabiyeen katika bango la Jalsa, akagundua kuwa masheikh wanaopinga Waahmadiyya wanasema uwongo kwamba Waahmadiyya hawaamini kuwa Mtume (s.a.w) ni Khaatamun Nabiyeen.

Vyombo vya Habari: Mitandao na idhaa za BBC (Regional) BBC South, BBC World, BBC National News, zimetangaza kwa kirefu tarifa za Jalsa Salana na ujumbe wa Jumuiya ukawafikia watu milioni 52.

Tovuti 40, Magezeti 20, Idhaa za Redio 16, Idhaa za Televisheni 12 zimetangaza taarifa na vipindi vya Jalsa Salana Uingereza.

Watu milioni 16 wamepata ujumbe kupitia mitandao ya kijamii.

Nchini Bangladesh katika eneo la Dhaka wageni 800 wasiokuwa Waahmadiyya walishiriki katika kusikiliza Jalsa Salana UK. Na vyombo 10 vya mitandao ya kijamii vilitangaza taarifa, hivyo watu milioni 5.4 wamepata ujumbe.

MTA INTERNATIONAL: Kupitia kituo cha YouTube cha MTA, zaidi ya watu milioni 15 walitazama shughuli za Jalsa, watu 35,000 walitembelea kupitia Instagram yao na zaidi ya 100,000 walitembelea ukurasa wao wa Twitter. Zaidi ya watu 550,000 walitembelea ukurasa wao wa Facebook pia.

Khalifa mtukufu (atba) kisha aliomba kwamba Jalsa iendelee kuleta matokeo mazuri na kuwezesha watu zaidi na zaidi kuelekeza mawazo yao kwa Uislamu wa kweli, na watu walindwe kutokana na uovu wa wale wanaoitwa makleri.

Kifo Juu ya msalaba? Hoja kumi kutoka kwenye Biblia Takatifu

Kuzaliwa (uzao) kwa Yesu

La ajabu ni kwamba wafuasi wa dini kuu tatu duniani yaani Wayahudi, Wakristo na

Waislamu wanatofautiana kuhusu kuzaliwa na kifo cha Yesu Kristo, aliyezaliwa miongoni mwa Mayahudi. Wanaitakidi kuwa kuzaliwa kwake kulikuwa ni kwa haramu na wanatoa masingizio dhidi ya Mariamu, mama yake Yesu. Wanamtangaza kuwa mwana haramu (Mungu apishe mbali) na hivyo kutostahili "kuwa katika mkusanyiko wa watu bwana".

Wakristo kwa upande mwingine wanaamini ya kuwa Yesu Kristo alizaliwa bila baba na hivyo akawa ni mwana wa Mungu. Hii inaonesha Wayahudi na Wakristo wana mitazamo tofauti iliyopita kiasi kuhusu kuzaliwa kwa Yesu.

Waislamu kwa upande

wao hawana shaka juu ya Yesu kuzaliwa bila baba, lakini sio mwana wa Mungu.

Kuzaliwa bila baba linaweza kuwa tukio la ajabu kidogo lakini sio kinyume na

maumbile. Ipo mifano katika historia ya utabibu inayoonesha kuwa mabikira walipata watoto. Hata Adamu anayekubalika kuwa mwanzilishi wa kizazi hiki cha sasa alizaliwa bila ya kuwa na baba wala mama.

Hii ni imani ya dini zote tatu tulizokwisha zitaja. Waislamu wanaamini kuzaliwa kwake bila ababa hakuna uhusiano wowote na kuwa mwana wa Mungu au utakatifu.

Alikuwa ni binadamu na sio zaidi ya hivyo. Yesu mwenyewe alijiita mwana wa Adamu katika Agano jipya.

Kifo cha yesu

Kifo cha Yesu halikadhalika ni swala lenye utata miongoni mwa Wayahudi, Wakristo na waislamu.

Wayahudi wanaamini kwamba Yesu alifia msalabani kwa sababu alikuwa Nabii Muongo. Jambo hili wanalitolea ushahidi kutoa kwenye Biblia, "na ikiwa mtu ametenda dhambi inayostahili kifo, na akifa na ukimuamba msalabani huyo amelaani na Mungu. (Mwanzo 21:22-23).

Sawa na imani yao Yesu alikuwa Nabii muongo, hivyo alifia msalabani ikiwa ni alama ya mtu aliyelaaniwa na Mungu. Wakristo wao wanaamini ya kuwa Yesu aliwambwa msalabani na akafa kifo cha laana. Paulo anasema: "Kristo alitukomboa katika laana ya Torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu maana imeandikwa amelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti" (3:13).

Lakini Kurani Tukufu inatangaza akuwa Kristo hakufa msalabani. Mwenyezi Mungu alimuepusha na kifo cha kusulubiwa kama alivyo wanusuru wapendwa wake kutokana kwenye mateso. Je Yona hakutoka mzima kutoka kwenye tumbo la nyangumi?

Ukweli ni kwamba Yesu Kristo alizimia pale msalabani, lakini alipoondolewa pale msalabani alirejewa na fahamu na baadaye akafa kifo cha kawaida akiwa na umri wa miaka 120 Kwa ushahidi mzito wa imani yao kuwa Yesu Kristo alikuwa nabii muongo Wayahudi hususana mafarisayo wa wakati wake walitunga masingizio mazito wa kisiasa ya kwamba hakua mtiifu kwa Mfalme wa Rumi na kwamba alikuwa amedai kuwa Mfalme wa Wayahudi. Gavana Pilato hakuamini kuwa Yesu alikuwa na hatia lakini kwa sababu ya hofu ya umati wa Wayahudi, alimtoa Yesu aende kusulubiwa.

Walimuweka msalabani, ambapo alikaa kwa saa tatu au nne tu na halafu akaondolewa akiwa katika hali ya kuzirai na kuwekwa kwenye pango lililokuwa kwenye shamba karibu na tukio.

Kifo kwa njia ya kusulubiwa kilikuwa kinachukua siku nyingi. Mtu aliyewekwa msalabani alikumbana na madhila ya njaa na kiu na aghalabu miguu yao ilivunjwa.

Walikufa kifo kilichochukua siku nyingi. Lakini haikuwa hivyo kwa Yesu Kristo.

Kama ilivyotokea, yeye aliwekwa msalabani Ijumaa alasiri na siku iliyofuata ikiwa ni Sabato siku ya wayahudi – hakuna mwenye hatia aliyeruhusiwa kuwa kwenye msalaba katika siku hiyo takatifu, hivyo aliondolewa pale msalabani baada ya saa tatu au nne.

Kupoteza damu kwa wingi kulimfanya zirai. Alidhaniwa ya kuwa amefariki. Mwili

wake uliwekwa kwenye pango lililokuwa kwenye bustani ya Yusufu wa Arimathaya ambaye alikuwa mwanafunzi wake. Yesu akiwa bado mzima katika pango

Endelea uk 10

Bustani ya Washairi

YANGA

1. Timu imechangamka, inataka ushindani
Shikalo anavyodaka, abilingika golini
Jafari aseleleka, kuzuia wapinzani
Yanga Africa yang›ara, piga pasi mpenyezo.

2. Lamine amezishika, kila tumu uwanjani
Hakubali kupitika, anapokua kazini
Kulia wamedhikika, watu wanapigwa pini
Yanga Africa yang›ara, piga pasi mpenyezo.

3. Kulia wamedhikika, shughuli ya mnyamani
Na maji yanamwagika, kumwagikia golini
Boksa kapumzika, atarudi uwanjani
Yanga Africa yang›ara, piga pasi mpenyezo.

4. Dante ana vibweka, na kati kuna Yondani
Striker wanakabika, hawaingii golini
Mipira inapenyeka, kuelekea dimbani
Yanga Africa yang›ara, piga pasi mpenyezo.

5. Mali inapokeleka, shishimbi weka gambani
Piga mtu mueleka, mpe fundi mjivuni
Na kanzu anawavika, piga tobo miguuni
Yanga Africa yang›ara, piga pasi mpenyezo.

6. Penseli inafika, weka mali kabatini
Hachelewi kukunjuka, kuelekea golini
Pasia enjoy soccer, piga chenga ya makini
Yanga Africa yang›ara, piga pasi mpenyezo.

7. Uncle anamwagika, kumuona Morrison
Nchimbi kwenye pilika, kuangalia golini
Tariki akainyaka, akanyooka golini
Yanga Africa yang›ara, piga pasi mpenyezo.

8. Piga pasi uhakika, na ifike mguuni
Makame acha vibweka, embu toka utotoni
Bado ni kinda kumbuka, waitajika dimbani
Yanga Africa yang›ara, piga pasi mpenyezo.

9. Feisal kubomboka, tumekumisi dimbani
Mita mia kufyatuka, unaingiza kimyani
Tunawindwa kwa hakika, tujitahidi jamani
Yanga Africa yang›ara, piga pasi mpenyezo.

10. Metacha umedhikika, unapokua golini
Waonekana kuchoka, unakosa umakini
Unaona heka heka, hauongei kwa nini?
Tariki acheze tisa, nchimbi acheze kumi.

11. Namba sita uhakika, Makapu baki uani
Ulivifanya vibweka, ulipocheza dimbani
Hukupanda ulishuka, ulikabia kwa chini
Tariki acheze tisa, nchimbi acheze kumi.

12. Kule mbele kadhalika, msilete ukatuni
Wawe wawili hakika, wataingiza nyavuni
Mmoja anapotoka, mwingine apiga pini
Tariki acheze tisa, nchimbi acheze kumi.

13. Yule Yipe kashachoka, hana kitu mguuni
Na molinga kadhalika, wafukuzeni chamani
Machozi yananitoka, Yanga mbele wanabuni
Tariki acheze tisa, nchimbi acheze kumi.

Abdallah Kalindima (K-mtoto)
MMAKONDE MSOMI

WOKOVU

1. Salamu Ndugu zanguni, kwa mola naegemea,
Alhamdu rahmani, nuru kwa kunangazia,
Nimezaliwa kundini, ahmad memjua,
Vitabuvye darasani, Mengi akanifumbua,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

2. Kuwekwa msalabani, na damu wakamtoa,
Si wokovu tambueni, mungu alishakataa,
Ismaili jangwani, mola alimkataa,
Kwa wahayi Wa ndotoni, kondoo akamtoa,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

3.kabla kufika mbeleni, akili yako tumia,
Wema Wa hapo zamani, dhambi vipi jizuia?
Kwa mungu kaa tumboni, au kafara jitoa!!
Hayo si ya kitabuni, Musa alotuambia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

4.wokovu siyo imani, Bali dhambi kukimbia,
Pata okoka dhambini, bada mola mtambua,
Wokovu msalabani, ulaya wameshikia,
Vipi pombe vilabuni, zinaa nako kuua?
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

5.busara zitumieni, waungwana kutambua,
Pombe mzizi dhambini, si matusi si zinaa,
Duniani chunguzeni, wapi iliko zagaa,
Kama si msalabani, wapi palipozidia?
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

6. Wokovu kweli ni nini!?, dhambini tao kutoa,
Mwenyezi mungu yakini, kwa hoja kumtambua,
Kwa dalili akilini, kumuogopa jalia,
Na Upendo Wa moyoni, pekee kumpatia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

7. Naswali kwa wanadini, vipi dhambi waingia,
Hali mnayo imani, ya mungu wetu rabia!,
Hamumuogopi manani, duniani natulea,
Hamumpendi rabani, pepo alo iandaa,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

8. Swali ninawajibuni, dhambi linaloibua,
Imani siyo yakini, ujinga pasi tambua,
Moyo ulo nayakini, dhambi haiwezi kaa,
Kama kutwa na gizani, pamoja wezi tulia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

9. Mfano tuoneni, kwa ubongo kutambua,
Jiwe lile mkononi, tiba kila maradhia,
Chafwata nini wadhani, kifua takumbatia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

10. Mfano tugeuzeni, huku tukifikiria,
Jiwe liwe mkononi, pasi wewe kutambua,
Kama lile mkononi, ni sumu yenye kuua,
Tabaki nalo wadhani, mbali utalirushia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

11. Umepata somo gani, kama umefikiria,
Kwa asili insaani, vizuri twajivutia,
Vibaya vya hatarini, hatutaki karibia,
Sasa kwanini dhambini, hatutaki kujitoa?
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

12. Enyi Ndugu wanadini, hakika yupo jalia,
Tafuta kweli yakini, dhambini hutojitia,
Utakuwa adhabuni, kila tendo kikosea,
Pakufikia Motoni, waovu wataingia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

13. Akili zitumieni, yakini kuitambua,
Mifano ya duniani, michache kuangalia,
Hutobaki kiburini, hatari kikuingia,
Mifano ya hapa chini, kwa busara angalia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

14. Je tautia motoni, mkono kifurahia?
Mlimani kileleni, chini tajiangushia?
Kwa hiyari kisimani, radhi utajitupia?
Kama si woga kwanini, hatari hutoingia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

15. Je utalala relini, gari moshi La kujia?
Mkono tia kinywani, mwa simba alo na njaa,
Hautotoka chumbani, moto ukikuwakia,
Hutoruka kitandani, nyoka ukimlalia?
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

16. Hatari za duniani, kwa woga utajitoa,
Vipi hatari mbinguni, kwanini wakurubia,
Umeikosa yakini, baya dhambi hujajua,
Heri kuwa mautini, si mola kumkosea,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

17. Za juu juu imani, sababu kuangamia,
Adhabu ilo Motoni, wanadhani ni mzaa,
Wadhani wameamini, mola wajamtambua,
Qiyama hawaamini, mola hatotufufua,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

18. Nimefika ukingoni, mwenye akili kajua,
Wokovu hasa ni nini, dhambi utakuokoa,
Mola ya kweli yakini, ndiyo Tiba maradhia,
Taokoka tambueni, peponi mtaingia,
Utambueni wokovu, dhambi upate ishinda.

Masihi Omary Kisagwa

DUNIA MAZIGAZI

Bismillahi azizi, Muumba maji na hewa,
Tujaze yako mapenzi, kila kitu kiwe sawa,
Tuvishe safi mavazi, tupendeze sawasawa,
Usione umepewa, dunia 'ltna.-.zigazi.

2. Natambua mbili kazi, insi tumepatiwa,
Haki ya Mungu Mwenyezi, kutimiza ndio dawa
Na viumbe kila ngazi, hakizo kutimiziwa,
Usione umepewa, dunia magazigazi.

3. Kitu nilicho maizi, na babu niliambiwa,
Dunia tangu na enzi, ina uwili nielewa,
Heshimu wako wazazi, mema utabarikiwa,
Usione umepewa, dunia magazigazi.

4. Tazama jua na mwezi, na nyota twamilikiwa,
Kodi Mungu hatutozi, ni bure twahudumiwa,
Ardhi yetu makazi, vingi tumependelewa
Usione umepewa, dunia magazigazi.

5. Kwa zama hizo na hizi, mengi tumehadithiwa,
Tangu vya kale vizazi, sicheke mwana mkiwa,
Yatima mla madanzi, mpe ukijaaliwa,
Usione umepewa, dunia magazigazi.

6. Leo chai kwa mruzi, kesho nyama na maziwa
Ulikuwa kijakazi, na leo muheshiwa,
Umefilisika juzi, leo unasimuliwa,
Usione umepewa, dunia magazigazi.

7. Kama mali na kizazi, tunu umetunukiwa
Na usiwe mchokozi, kwa ulichobarikiwa,
Huenda mikia mbuzi, bado hujasitiriwa,
Usione umepewa, dunia magazigazi.

8. lla uliye machozi, kama dini hujapewa,
Umtii kiongozi, Masihi Muahidiwa,
Ni utajiri wa wazi, ukwasi usojutiwa,
Usione umepewa, dunia magazigazi.

9. Na uwapo kiongozi, usije sifa kulewa,
Sikiza wenye machozi, ndugu umeaminiwa,
Dunia mengi masizi, usije kuhadaiwa,
Usione umepewa, dunia magazigazi.

l0. Ni mwisho wa kuperuzi, bunge tumesitishiwa,
Tumepata maamuzi, naondoa hili siwa,
Tumshukuru azizi, kwa tulichokadiriwa,
Usione umepewa, dunia magazigazi.

Mwl. Najat Fakim Said. Nang'olo
THE BIG BOSS
KINEGEMBASI - IRINGA.

YALIYOPITA SI NDWELE

Bado nafasi unayo, sikae bali SIMAMA
Makovu katika moyo, ni bado yanakuchoma
Shime yasahau hayo, yanachafua mtima
Yaliyopita si ndwele, ugange yanayokuja

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)
Kiwalani - Migombani

Mzee na Vijana wake wanne

Mzee mmoja alikuwa na wana wanne. Alitaka wanawe wajifunze kutokuhukumu chochote haraka sana. Kwa hivyo aliwatuma kila mmoja kwenye jukumu, kwa zamu kwenda kutazama mti wa mpea ambao ulikuwa mbali sana. Mwana wa kwanza alienda katika msimu wa baridi. Wa pili katika msimu wa masika. Wa tatu katika msimu wa kiangazi. Na mdogo kabisa wakati wa msimu wa kipupwe. Wote walipokwisha kutembelea



na kurudi, mzee huyo aliwauliza wanawe kuelezea mti wa mpea.

Mwana wa kwanza alisema mti huo ulikuwa mbaya, umeinama na umesokota. Mwana wa pili akasema hapana, ulikuwa umefunikwa na vichipukizi vya kijani kibichi na unakaribia kuzaa. Mwana wa tatu alikubaliana na kaka zake na akasema ulikuwa umejaa maua na harufu tamu na ulionekana mzuri sana kwa msimu mmoja tu.

Mzee alisema wote wako sawa, kwani waliuona mti katika msimu mmoja mmoja tu. Akawaambia kuwa hawawezi kuuhukumu mti, au mtu, kwa msimu mmoja tu. Dhati ya wao ni nani na raha, furaha na upendo ambayo hutokana na maisha inaweza kupimwa tu mwishoni, wakati misimu yote imeisha. Ukikata tamaa na msimu mmoja, utakosa ahadi ya masika, uzuri wa kiangazi na utimilifu wa mavuno. Aliwaambia wasiruhusu maumivu ya msimu mmoja yapoteze furaha ya wengine wote.

Usihukumu maisha kwa msimu mmoja mgumu, vumilia kupitia viraka vigumu na nyakati bora hakika zitakuja baadaye.

TAFUTA MANENO

Yatafute maneno 30+ hapo chini kwa kuyazungushia na Penseli

J	Y	C	L	H	M	X	F	Z	K	C	K	W	M	M	D	W	L	H	R	K	Q
K	G	G	R	A	G	Y	B	R	D	A	B	D	U	L	L	A	H	N	Z	P	K
M	B	D	L	C	Z	R	K	W	R	Y	M	J	Z	L	L	J	N	L	N	H	V
Y	G	S	D	H	P	R	D	J	R	M	Y	H	H	A	F	I	D	H	C	K	T
V	I	B	C	A	C	Y	T	L	F	D	P	K	A	X	H	S	N	B	B	K	I
L	M	R	R	D	L	R	Z	M	R	B	A	H	J	D	L	J	A	H	K	L	B
C	H	L	T	I	T	K	T	C	J	J	S	X	P	R	H	S	N	L	I	Y	T
G	V	I	F	T	K	R	C	M	I	L	A	X	L	M	F	R	U	D	A	T	N
R	Q	R	J	H	T	T	R	D	T	Q	H	C	H	T	T	G	A	N	N	T	A
F	X	Q	A	A	V	T	A	R	T	Y	A	V	M	F	P	R	W	T	N	B	D
Q	M	Z	B	M	B	H	N	Y	R	F	B	Q	U	B	L	X	P	R	R	A	H
Z	N	F	U	M	K	Y	L	M	L	N	A	P	B	R	J	G	Z	P	X	Z	A
R	P	W	B	K	J	A	M	A	A	A	M	L	A	R	A	B	U	W	A	P	N
C	Q	J	A	D	Q	C	T	G	N	T	B	R	H	R	Y	K	T	H	R	G	A
Q	W	I	K	Z	T	X	R	T	Q	C	N	A	A	N	M	Y	S	N	H	M	D
X	H	B	A	W	T	K	M	L	X	J	B	Z	L	W	M	I	V	N	Z	W	I
R	A	R	R	T	D	N	V	P	X	A	H	M	A	D	A	M	A	Q	J	N	W
P	S	A	Y	R	T	J	H	Z	A	V	T	M	Z	I	W	J	F	M	I	L	H
Q	I	H	V	Q	J	A	M	K	W	L	B	Y	F	N	H	G	Q	D	I	Y	P
N	D	I	J	C	L	A	T	N	N	R	K	Z	R	K	M	S	R	Z	F	N	G
H	I	M	M	L	R	P	M	M	F	Z	C	M	A	D	I	N	A	Z	Q	T	A
N	K	F	A	L	B	T	W	A	D	C	L	X	X	T	N	T	T	N	N	C	B
R	N	Q	J	P	L	J	C	T	A	T	K	R	N	M	U	H	A	M	M	A	D
K	F	T	Y	A	T	H	R	I	B	T	V	H	Z	M	K	Y	N	Q	K	J	Z

UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.



Jinsi ya kupika Keki ya Nazi

Na **Mtandao**



VIPIMO
1. Unga ½
2. Kikombe cha Sukari ½
3. Kikombe cha mayai ¼
4. Baking powder ½ kijiko cha chai
5. Maziwa kiasi tuu & Tui la Nazi
6. Vanilla ½ kijiko

NAMNA YA KUPIKA KEKI
1. Tia siagi sukari na baking powder piga kutumia mashine(mchapo) mpaka iwe laini
2. Tia mayai na uendelee kupiga
3. Tia unga polepole huku ukiendelea kuupiga ongeza na tui la nazi
4. Tia maziwa na vanilla piga kidogo tumia treya ya vishimo(muffin tray) weka karatasi zake kisha mwaga ule mchanganyiko katika vishimo kiasi kiasi chunga usivijaze sana
5. Choma(bake) katika moto wa 325°c kwa dakika 10-15 mpaka iwe rangi ya uthurungi(brown)
6. Epua Hapo itakuwa Tayari kuliwa

NB; kama haujazoea kulamba lamba vidole bora usipike.

NUKUU YA HADITHI

Na **Ustadhi Issa Malenge** - 0625 914 740 0752 334 332

حَدَّثَنَا أَبُو بَكْرِ بْنُ أَبِي شَيْبَةَ حَدَّثَنَا عَبْدُ اللَّهِ بْنُ إِدْرِيسَ عَنْ يَحْيَى بْنِ سَعِيدٍ وَعُبَيْدِ اللَّهِ بْنِ عُمَرَ عَنْ عُبَادَةَ بْنِ الْوَلِيدِ بْنِ عُبَادَةَ عَنْ أَبِيهِ عَنْ جَدِّهِ قَالَ بَايَعْنَا رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَلَى السَّمْعِ وَالطَّاعَةِ فِي الْعُسْرِ وَالْيُسْرِ وَالْمَنْشَطِ وَالْمَكْرَهِ وَعَلَى أَثَرَةٍ عَلَيْنَا وَعَلَى أَنْ لاَ نُنَازِعَ الأَمْرَ أَهْلَهُ وَعَلَى أَنْ نَقُولَ بِالْحَقِّ أَيْنَمَا كُنَّا لاَ نَخَافُ فِي اللَّهِ لَوْمَةَ لاَئِمٍ

Imesimuliwa na Hadhrat Abul Walid Ubada bin Swamit r.a. aliyesema:
Tulifanya baiat kwa Mtume s.a.w juu ya sharti kwamba tutasikia na tutatii katika dhiki na faraja. Katika furaha na karaha. Na hata kama wengine watapendelewa kuliko sisi.
Na kwamba hatutagombana na wenye mamlaka isipokuwa tukiona kufuru bayana ambayo juu yake tunayo hoja kutoka kwa Mwenyezi Mungu.
Na kwamba tutasema kweli tupu popote tulipo bila kuogopa lawama ya mwenye kulaumu kumhusu Mwenyezi Mungu. (Bukhar).

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA as
Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w

Nuru tukufu aliyojaaliwa mtu yaani yule mtimilifu zaidi miongoni mwao, haikugawiwa malaika, wala nyota, wala haikuwemo mwezini au juani, au katika bahari na mito; haikuwa ipatikane katika vitu vya zumaradi au lulu n.k.; haikuwemo katika kitu cho chote cha ardhini au mbinguni.
Nuru hii alikuwa nayo mtu mkamilifu peke yake, ikadhihirika kwa njia timilifu kabisa katika dhati ya Bwana wetu na Kiongozi wetu, Muhammad Mtukufu, mbora wa Manabii wote, kiongozi wa wale walio hai (machoni pa Mungu). Hivyo basi, ile nuru tukufu akaipata mtu yule kikamilifu kabisa, na vivyo hivyo, kwa kiasi fulani, wakapewa wale wote ambao katika baadhi ya hali zao, walifanana naye .... Neema tukufu katika dhihirisho lake timilifu zaidi akaipata Bwana wetu na Kiongozi wetu, Nabii asomjuzi wa kusoma wala kuandika, mkweli, ambaye uaminifu wake washuhudiwa, Muhammad mteule, amani na baraka za Mwenyezi Mungu juu yake.
(Roohani Khazain Jal. 5, Uk. 160-162: Aaina Kamalat-e-Islam Uk. 160).

DARASA LA QUR'AN TUKUFU

Haiwezekani Qur'an Tukufu Kutungwa na Binadamu

Na **Musa Salum Mgeleka -** 0717 504 690

وَمَا كَانَ هَٰذَا الْقُرْآنُ أَنْ يُفْتَرَىٰ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَلَٰكِنْ تَصْدِيقَ الَّذِي بَيْنَ يَدَيْهِ وَتَفْصِيلَ الْكِتَابِ لَا رَيْبَ فِيهِ مِنْ رَبِّ الْعَالَمِينَ
Na haiwezekani Qur›an hii kutungwa na ye yote isipokuwa Mwenyezi Mungu. Bali inayasadikisha yaliyo mbele yake, na ni maelezo ya Kitabu. Haina shaka, imetoka kwa Mola wa walimwengu. Surah 10:38

Qur›an katika Aya hii inatoa sababu tano zenye nguvu sana kuonyesha ya kwamba bila shaka imetoka kwa Mwenyezi Mungu, na haikutungwa na mwanadamu.
1. Hoja ya kwanza inayodokezwa na maneno, isipokuwa Mwenyezi Mungu, ni ya kwamba Qur›an ina habari za namna ambayo zimekiuka akili ya mwanadamu kuzijua, na haziwezi kubainishwa ila na Mwenyezi Mungu peke yake. Sasa katika mambo yanayojulikana na Mwenyezi Mungu peke yake, ni habari za mambo ya ghaibu, kama bishara zinazotaja matukio makubwa ya baadaye; na hapawezi kuwa shaka juu ya Kitabu kutoka kwa Mungu chenye habari anazozijua Mungu peke yake.
2. Hoja ya pili inayotolewa hapa kuonyesha kuwa Qur›an imetoka kwa Mwenyezi Mungu ni kwamba mbali na bishara zake yenyewe, kubatilisha wazo la kusema imetungwa na mtu, bishara za Manabii waliotangulia pia zinahakikisha kuwa Qur›an imetoka kwa Mungu. Jambo hili linagusiwa katika maneno haya, inayasadikisha yaliyo mbele yake, na ni wazi ya kwamba hakuna kitabu kinachotungwa na mwanadamu kinachoweza kujitimizia bishara zilizotabiriwa katika Vitabu vya Manabii waliopita zamani.
3. Hoja ya tatu iliyomo katika Aya hii inagusiwa na maneno haya Maelezo ya Kitabu, yaani Qur›an inaeleza na kutoa tafsiri ya mafundisho ya Vitabu vya zamani. Hii pia ni dalili yenye nguvu sana ya ukweli wa Qur›an. Vitabu vilivyotangulia vinahitaji msaada wa Qur›an kwa kufafanua mafundisho yao. Taurati, Injili, Vedas, Zend-Avesta - vyote hivi ni vitabu vya zamani vinavyoshughulika kueleza mafumbo makubwa makubwa ya mambo ya dini kama vile umoja wa Mwenyezi Mungu, wahyi na ufunuo, sifa za Mwenyezi Mungu, utume, maisha ya Akhera, hali za tabia na za roho n.k.w. Lakini hakuna kimoja katika vitabu hivyo kinachoeleza mambo haya kwa namna ya kuyafanya yawe wazi kabisa na kufahamika, na mitatanisho yao ni lazima ielezwe kwa msaada wa mafundisho ya Qur›an.
Hivyo Aya hii inaleta madai ya kwamba Qur›an inaeleza na kufafanua sehemu za vitabu vya zamani zisizofahamika vyema na zenye kutatiza; na makafiri wanaambiwa ya kwamba kama watakataa Qur›an kutoka kwa Mungu, watalazimika kukubali ya kwamba Mungu mwenyewe hakuweza kutia elimu nyingi ya mambo ya kiroho katika Vitabu vya zamani kama alivyoweza mwanadamu (Mtume Muhammad) kufanikiwa kutia katika hiki Kitabu kidogo tu cha Qur›an. Hivyo wafuasi wa dini nyingine watalazimika ama kukubali Qur›an imetoka kwa Mungu au kukataa Vitabu vya zamani pia.
4. Hoja ya nne katika Aya hii imo katika maneno, Haina shaka, yaani Qur›an ina hoja zote na dalili zote zinazotakikana kuthibitisha kuwa imetoka kwa Mungu, na haina haja ya kusaidiwa na mtu nje au kitabu kingine kwa jambo hilo. Qur›an inaeleza migogoro ya maisha ya watu kukaa pamoja, ya mwenendo na tabia na ya mambo ya kiroho, kwa ukamilifu na utoshelezo wa namna ambayo mtu ye yote atakayeifikiria bila upendeleo ataona mara moja ya kuwa Qur›an haitoi madai yo yote ila inayafuatisha na hoja madhubuti, na dalili imara. Jambo hili ni ushahidi usiokanushika ya kwamba Kitabu hiki bila shaka kimetoka kwa Mungu; maana Qur›an inataka tuamini mambo mengi yasiyoonekana, na haiko katika uwezo wa mwanadamu kuhakikisha mambo yasiyoonekana kwa hoja za akili tu bila kusaidiwa na uwezo wa kutazama na mazoea. Lakini ni wazi mtu hawezi kuviangalia vitu visivyoonekana na kuvizoea. Mungu tu ndiye awezaye kufanya hivyo.
5. Hoja ya tano ya kuhakikisha kuwa Qur›an imetoka kwa Mungu inayoelezwa na Aya hii imo katika maneno haya, Imetoka kwa Mola wa walimwengu. Maneno haya yanadokeza ya kwamba kwa Qur›an hii sifa ya Mwenyezi Mungu ya Rabbul ‹Aalamiin (Mola wa walimwengu) imedhihirishwa kwa wanadamu wote. Qur›an haikusudiwi kutosheleza mahitaji ya taifa mojawapo au majira fulani tu, kama ilivyokuwa hali ya Vitabu vilivyotangulia; bali inakusudiwa kutosheleza haja za mataifa yote na za nyakati zote. Kwa hakika haiwezekani kwa mwanadamu kutoa Kitabu kinachoweza kutosheleza haja za wanadamu wote kwa nyakati zote. Kwa desturi mtu huvutwa na mastakimu yake naye huangalia na kutaka kutosheleza haja zake zilizo karibu naye. Ni Mungu peke yake anayeweza kutoa mafundisho ya namna ambayo yawe yanafaa sawasawa kila wakati na kwa watu wote, ambayo hayawezi kuhafifishwa na mabadiliko ya nyakati na hali. Basi Qur›an ndiyo ina mafundisho ya namna hiyo.

Mola wetu, tumiminie uvumilivu na Utufishe watii/ Waislamu. Amin

MATUKIO KATIKA PICHA



Sheikh wa Mkoa Shinyanga alishiriki mkutano maalum iliyoandaliwa na ofisi ya Mhe DC Shinyanga. Mgeni Rasmi alikuwa Mhe. Mkuu wa Mkoa na Katibu Twala pia alikuwepo. Viongozi wengine wa dini mbalimbali na serikali pia walishiriki hafla hii.



Khalifatul Masih Vatba akihutubia kipindi cha ufungaji cha Jalsa Salana (mkutano wa mwaka) ya Uingereza 2021



Shindano la Usomaji wa Mashairi katika Jamia Ahmadiyya Tanzania



Muonekano wa angani wa kiwanja cha Hadiqatul mahdi palipofanyika mkutano wa mwaka wa Uingereza 2021



Muonekano wa angani wa Khuddam katika mkutano kwa mtandao na Hazrat Khalifatul Masih V (atba) katika Ijtimaa ya Majlis Khuddamul Ahmadiyya Ujerumani - 22 Agosti 2021



Banda la Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania katika Maonyesho ya Vitabu yaliyofanyika katika Viwanja Vya Makumbusho ya Taifa Dar es salaam tarehe 26-28 Agosti 2021



Banda la Majlis Ansarullah Ahmadiyya Tanzania katika Maonyesho ya Vitabu yaliyofanyika katika Viwanja Vya Makumbusho ya Taifa Dar es salaam tarehe 26-28 Agosti 2021

اعجاز المسیح - Muujiza wa Masihi



Na **Sheikh Muzaffar Durrani**
Rabwah, Pakistan

Kutoka uk. 1

na kudai kwamba mtu ambaye hajui hata lugha ya Kiarabu, lugha ya sheria ya dini ya Kiislamu, atawezaje kufundisha na kuongoza Uislamu.

Seyidna Ahmad[as] kwa kweli, hapo kabla hakujua lugha ya Kiarabu kiasi cha kutosha. Kwa hiyo alimuomba Mwenyezi Mungu aliyemtuma kwamba apewe jibu la swali hili na afundishwe lugha ya Kiarabu. Na kweli ikatokea hivyo hivyo. Seyidna Ahmad[as] alitangaza kwamba Mwenyezi Mungu amemfundisha mizizi elfu arobaini (40,000) ya maneno ya asili ya lugha ya Kiarabu katika usiku mmoja tu. Hilo lilikuwa sio tu tangazo tupu, bali baada ya hapo Seyidna Ahmad[as] aliandika vitabu 25 katika lugha ya Kiarabu akieleza masomo ya dini. Sasa akawaita wapinzani hao waje washindane naye kwa ufasaha na ujuzi wa lugha ya Kiarabu.

Seyidna Ahmad[as] alileta maoni mazuri kwamba badala ya kushindana kwa njia nyingine, tushindane katika kuandika maelezo ya Kurani Tukufu katika lugha ya Kiarabu na tuyachapishe. Kwa njia hii itajulikana kwamba nani anajua lugha ya Kiarabu na nani anapiga makelele ya bure. Pia kwa kupatikana maelezo ya Kurani watu watafaidika nayo. Hapo masheikh wote wakanyamaza. Seyidna Ahmad[as] akawajulisha na kuwakumbusha mara kwa mara lakini wote wakakwepa.

Kisha Seyidna Ahmad[as] akawambia masheikh kwamba: Enyi masheikh wa India, mnaweza kujumuika na masheikh wa nchi za Misri, Shamu na Uarabuni. Kisha njooni nyote kwa pamoja tuandike maelezo ya Kurani. Wakati Seyidna Ahmad[as] alipoona kwamba bado hawapati ujasiri wa kukabiliana naye, basi akaamua kuwarahisishia kazi, ili wapate ujasiri wa kuingia katika mapambano ili ukweli wa mambo udhihirike. Hapo akawambia kwamba kama mnaona kutoa maelezo ya Kurani nzima ni jambo kubwa sana na gumu, basi tushindane kuandika tu maelezo ya sura moja tutakayoichagua kwa njia ya kura. Lakini hata hivyo hakuna Sheikh yeyote aliyejitokeza, ingawa hapo awali walijigamba sana na kupiga makelele.

Mwishowe Seyidna Ahmad[as] akatangaza kwamba mimi nimewakaribisheni sana katika mashindano haya, lakini hadi sasa sijapata jibu lolote kutoka kwa Sheikh yeyote yule. Sasa mimi mwenyewe nimeamua kuchagua Suratul Faatiha na kuyaandika maelezo yake kwa jina la Ijazul Masihi.

Kwa hiyo akaandika na kukichapisha kitabu hiki mnamo tarehe 20.02.1901 na aliwapelekea kitabu hicho wapinzani kwa njia ya posta rejista. Akatoa hata changamoto ya kumtaka mwanazuoni yeyote aandike mfano wa kitabu hiki.

Baada ya kupata bishara kutoka kwa Allah, Juu ya jalada la nje la Kitabu hicho akaandika hivi:

اِنَّهٗ كِتَابٌ لَيْسَ لَهٗ جَوَابٌ مَنْ قَامَ لِلْجَوَابِ وَ تَنَمَّرَ ۔ فَسَوْفَ يَرٰى اَنَّهٗ تَنَدَّمَ وَ تَذَمَّرَ

Yaani ***hiki ni kitabu kisichojibika. Mtu yeyote atakayesimama kukijibu na kujiandaa kufanya hivyo, bila shaka atajikuta akiwa ni mwenye majuto, aliyefedheheka na kuangamia.***

Tena Seyidna Ahmad[as] alisema kwamba wanazuoni hawataweza kuleta mfano wake. Mwenyezi Mungu atazivunja kalamu zao na kuziharibu akili zao wasiweze kuandika mfano wa kitabu hiki (uk.37). Hata kama wajumuike na wasaidiane mababa zao, wana wao, wenzao, masheikh wao, wenye akili wao na mafakihi wao kuleta mfano wa maelezo ya Suratul Fatiha kama hayo ndani ya muda maalumu uliopangwa, hawataweza kamwe kuleta mfano wake, hata kama wasaidiane wao kwa wao. (uk.55)

Hakuna Sheikh yeyote aliyediriki kujitokeza kuleta mfano wa kitabu hicho kiitwacho Ijazul Masihi mbele ya Mjumbe na simba huyu wa Allah katika muda wake maalumu, wala katika uhai wa Seyidna Ahmad[as] wala katika miaka 120 iliyopita hadi leo.

Kama iulizwe kwamba je, kuandika kitabu ni muujiza, ilhali watu wanaandika vitabu kila siku? Basi jawabu lake ni kwamba kuandika kitabu si kitu lakini kuandika kitabu kwa njia ya mashindano, na kutangaza kabla kwamba Mwenyezi Mungu Amenipasha habari mapema kwamba hakuna mtu yeyote anipingaye atakayeweza kuandika kitabu cha aina hiyo na kisha kusisitiza kwamba kamwe hawataweza asilan kufanya hivyo na yeyote atakayejaribu na kudiriki kufanya hivyo, Mungu Ataivunja kalamu yake isiweze kudiriki kukubali changamoto hiyo na hatimaye itokee hivyo hivyo kwamba wapinzani wote washindwe kufanya hivyo, huo unakuwa tu ni muujiza uliothibitika kwa viwango vyote, hata kama makafiri watake au wasitake.

Twajua kuwa Mtume Mtukufu Muhammadsaw alipewa Kurani Tukufu ambayo kwa dhahiri ni kitabu tu, lakini Mwenyezi Mungu Aliwatupia wapinzani tambio kwamba:

وَ اِنْ كُنْتُمْ فِيْ رَيْبٍ مِّمَّا نَزَّلْنَا عَلٰى عَبْدِنَا فَاْتُوْا بِسُوْرَةٍ مِّنْ مِّثْلِهٖ وَادْعُوْا شُهَدَآءَكُمْ مِّنْ دُوْنِ اللّٰهِ اِنْ كُنْتُمْ صٰدِقِيْنَ

Na ikiwa mna shaka kwa hayo Tuliyomteremshia Mtumishi wetu, basi leteni sura iliyo mfano wa hii, na muwaite wasaidizi wenu ghairi ya Mwenyezi Mungu ikiwa mnasema kweli. (Al-Baqara, 2:24)

Pia Alisema kwamba:

قُلْ لَّئِنِ اجْتَمَعَتِ الْاِنْسُ وَ الْجِنُّ عَلٰٓى اَنْ يَّاْتُوْا بِمِثْلِ هٰذَا الْقُرْاٰنِ لَا يَاْتُوْنَ بِمِثْلِهٖ وَ لَوْ كَانَ بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ ظَهِيْرًا

Sema: Kama wajikusanye watu na majinni kwa kuleta mfano wa Kurani hii, hawataweza kuleta mfano wake hata kama wasaidiane wao kwa wao. (Banii Israaiil, 17:89)

Yaani Mtume Mtukufu Muhammadsaw alipewa Kitabu cha Kurani Tukufu. Wengine wote waliambiwa kuleta mfano wake lakini walishindwa kufanya hivyo. Kwa njia hii Kurani imekuwa ni muujiza mkubwa wa Mtume Muhammad[saw].

Vile vile Seyidna Ahmad[as] alipewa muujiza wa kutoa maelezo ya kina ya Kurani Tukufu. Akaeleza na kuandika maelezo ya Suratul Fatiha lakini wengine wote walishindwa kuleta mfano wa aina hiyo. Na ndio sababu akakiita Kitabu hicho kwa jina la Ijazul Masihi yaani Muujiza wa Masihi Mau'udi.

Waheshimiwa wasomaji, Wakati makafiri walipoitwa kuleta mfano wa Kurani Tukufu, wakajigamba hivi:

وَاِذَا تُتْلٰى عَلَيْهِمْ اٰيَاتُنَا قَالُوْا قَدْ سَمِعْنَا لَوْ نَشَآءُ لَقُلْنَا مِثْلَ هٰذَا اِنْ هٰذَآ اِلَّآ اَسَاطِيْرُ الْاَوَّلِيْنَ

Yaani ***wanaposomewa Aya zetu, husema: Tumekwishasikia. Tungetaka bila shaka tungesema kama haya. Haya si chochote ila ni hadithi tu za watu wa kale.*** (Al-Anfaal, 8:32)

Hivyo ndivyo wapinzani wa Seyidna Ahmad[as] tangu miaka 120 wanatapatapa tu kwamba 'Ijazul Masihi' si chochote, waweza tu kuandika mfano wake. Vile vile wanakosoa kosoa tu na wakifuata nyayo za makafiri wanatuhumu kuibia maneno ya vitabu vya zamani. Lakini ukweli ni huu kwamba wapinzani wote wa zama zote wa Seyidna Ahmad[as] wameshindwa vibaya sana kuleta mfano wa Ijazul Masihi. Huo ni msaada mkubwa kwetu na pigo kubwa kwa wapinzani kutoka kwa Allah sub'hanahu wa ta'alaa. Mwenye macho, na aone. Mwenye masikio, na asikie.

اِسْمَعُوا صَوْتَ السَّمَآءِ جَآءَ الْمَسِيْحُ جَآءَ الْمَسِيْحُ

Ndugu zangu wapendwa, ***Isikilizeni sauti ya mbingu kwamba Masihi ameshafika, Masihi Mau'udi ameshafika.***

Kifo Juu ya msalaba? Hoja kumi kutoka kwenye Biblia Takatifu

Kutoka uk. 5

lile alitoka katika pango (kaburi) lile siku ya tatu ilhali amejificha.

Akakutana na wanafunzi wake mahali panapoitwa Galileya na akala nao chakula. Vidonda vyake viliponeshwa na dawa ya kuchua ambayo ilikuwa imetayarishwa mahsusi na wanafunzi wake. Hii ndiyo hadithi ya kusulubiwa kwa Yesu. Maelezo ya wak juu wa kifo chake sio tu kwamba ni kinyume na maumbile bali ni kinyume pia na ushahidi wa historia na mantiki. Wanaamini ya kuwa Yesu hasa alifia msalabani na siku ya tatu alipaa kwenda mbinguni. Lakini ikithibitishwa kwamba hakufa msalabani na wala hakufufuka kutoka wafu basi msingi mzima wa Imani ya Kikristo unavunjika. Paulo ambaye ndiye hasa mwanzilishi wa ukristo kama tunavyo ufahamu hivi leo anasema: "Tena kama Kristo hakufufuka, basi kuhubiri kwetu ni bure na imani yetu ni bure. (Wakorintho 15:14).

Hayati Dr. Zwemar mmishionari maarufu wa Kimarekani anasema: "*Kama imani yetu juu ya kifo cha Kristo si sahihi basi ukristo mzima ni uongo mtupu*"

Itaendelea toleo Lijalo

Kwa nini *Biblia Ni Jibu* Wanamkana Nabii Issa kuwa Si Yesu?

Na **Juma Iddy Abeid,** Kigoma

Inaendelea Kutoka toleo lililopita

KIFO CHAKE

Yesu: Wanasema Tusomapo maandiko matakatifu ndani ya Biblia tunatambua kuwa Yesu alikufa na akafufuka na kwa kifo hicho kila zaminie atakombolewa. YOHANA 19:30-32: *Basi Yesu alipokwisha kuipokea ile siki alisema imekwisha akainama kichwa akai salimu roho yake . Basi askari wakaenda wakawa vunja miguu wakwanza na wapili alie surubiwa pamoja nae. Lakini walipo mjia Yesu na kuona ya kua amekwisha kufa hawa kumvunja miguu*.

Hoja yao hapo wakasema "Biblia inathibitisha kifo cha Bwana Yesu. Hapo ni sasa Issa hakufa ni wazi watakuwa ni wawili tofauti kwa sababu kama ingekuwa Issa ndie Yesu, basi tusingeona tofauti yao yaani kama maandiko yanayosema Yesu alikufa na kufufuka basi hata Issa angekuwa hivyo hivyo hawa ni wawili tofauti kwa sababu kama ingekuwa Issa ndie Yesu, basi tusingeona tofauti yao yani kama ingekuwa Issa ndie basi tusingeona tofauti yao yaani kama maandiko yanayosema Yesu alikufa na kufufuka basi hata Issa angekuwa hivyo tofauti na Yesu Mwokozi"

Hebu Tumtazame Issa;

Qurani 4:157 na kwa kusema kwao sisi tumemua Masihi Issa mwana wa Mariyam. Mtume wa Mwenyenzi Mungu nao hawakumua wala wawakumsulubisha bali walifananishwa au na hakika walio khitilafihana ujuzi nayo wowote , Ila ni kufuata dahana wala hawakumua kwa yakini.

Kwa hiyo kitabu hicho kinaeleza jinsi ambayo Issa hakufa au kwamuji wa kitabu hicho Issa alichukualiwa kwenda kwa Allah bila kuuwawa hivyo Issa hakufa.

Hapo Biblia inathibitisha kifo cha Bwana Yesu. Sasa na Issa hakufa, ni wazi kwamba watakuwa ni wawili tofauti kwa sababu kama ingekuwa Issa ndie Yesu, basi tusingeona tofauti yao yani kama maandiko yanavyo sema Yesu alikufa na kufufuka basi hata na Issa angekuwa hivyo hivyo. Hawa ni wawili tofauti mwisho wa kunukuu.

Uwe kweli *Biblia ni jibu* wamefungia ushindi wao wa tofauti ya Issa na Yesu Ukweli ukitazama kwa makini utaona tofauti yao katika madai ya kifo cha kufa na kufufuka kw kuhuwawa.

Lakini kama nilivyo sema kwa tatizo sio Qurani ila tatizo ni Biblia kuwa na Yesu Zaidi ya mmoja. Hivyo kuilaumu Qurani ni kutoitendea haki nayo hakuwa sifa ya watu wasio na busara kwani busara ni sifa yakupata habari tu busara ni siofa ya kupata habari na sitopata habari tu ila uwezo na kuzichuja Qurani hapo hapo katika tuko la Issa imetwaa kama hata mua hakumu ni mtu anayeweza kutoa usahi wa jambo ni kwa wakati wsahihiwa jambo hilo ni mpaka asitie Madai na ushahidi

Ndio kusema busara kwa walio jaliwa kuanza kupokea kwa madai ana habari gani juu ya madai yake.

Je utetezi unasemaje mwisho Ushahidsi au Mashaidi wanasemaje. Ukilielewa hilo hata wewe utakubali kuwa Hakimu ni lazima awe mwenye busara.

Yani hakimu nilazima apate maelezo ambaye ndio habari na ndipo aweze kuhukumu.

Issa - ni sifa ya yaliyosoma kufikia ukomo wa kujiengua kwa ufugaji wanajua unapovunja yai la hivyo ukuta ule mweupe ukiwa umelizunguka Goroli lenye mchanganyiko wa njano ya asifa na edamu ya chanzo cha kiumbe, ambalo *Biblia ni jibu* wakasema ni zeru zeru, huo ni upofu na kipofu wakasalimika yai hilo halikuwa kwa kuku bali kwa Mariyamu. Na ndio maana watu waliojiridhisha kuwa Mariyamu hakuwa Malaya wala Muasharati walipomuona Yesu walimwita Issa bin Mariyam (neno BIN ni chanzo) yaani ni chanzo cha yai lake mwenyewe Mariyamu.

Wakristo wao wakamwita Yesu yani sifa ya kuokoa ni sawa na kusema tu yai la Mariyamu ndio linalowaokoa.

Hivyo hapo Qurani ikaona ni mtu mmoja tu.

Isitoshe kwa kuwa mlengwa ni Mariam kuwa mama wa vitabu vya Luka na Mathayo vyote vilimlenga yeye. Hivyo Quran ikawaengua waume wa bandia wote Issa sio wa Luka wala Mathayo na ikampa haki yaani Mariyam. Hoja ya nasaba imejitiya yenyewe hapo.

Mada ya pili Mariyam huyo kuwa dada wa Haruni.

Je Mariyam huyo hakuonekana kwa Elizabeti? Je hakuwa katika nyumba ya Yuda pili hakuwa ndungu wa Haruni? Kwa kuwa Mariyam alikimbia kwa Elizabeti ili asipigwe mawe kwa kuzini na akaenda kwa ndugu yake. Qurani ikamwita na yeye ni ndugu

Kupitia kwa Elizabeti Quran hapo kosa lake nini? Bila shaka *Biblia ni jibu* ndio waficha ukweli na sio kweli eti Issa sio Yesu. Kwa unasaba wa Haruni. Lakini hata waumini wao Huenda wakawa na matatizo ya kutojiuliza Mfano mathayo amemuua Yesu na uzao wake mpaka kwa Adam. Swali hapo kuuliza kama Mariyam alikuwepo tena na Mariyamu na Adam Adam walitana vipi.

Hapo hoja ya Luka imeungwa mkono na kurani kua Mariyam ni dada wa Haruni na hakuwa Malaya wala asharati. na Inaonesha Huko kwa elizabeti ndipo alipo pata shutuma hizo

Hoja ya mwisho ndio kutokufa msalabani kwa Issa. wakati Yesu alikufa

Quran Tukufu imeona:

(1) Hawakumua msaalabani
(2) Hawakumsulubu
(3) Hawakuwa na uhakika nalo
(4) Hawakumuuwa

Swala la msingi ni kutazama vigezo vya Qurani hakimu ilitumiwa hekima gani. Busara (habari) zilikuwa zipi

(1) Mdai Yesu- alisema kwamba wapinzani wake atakuwa kama Yona. katika tumbo ola nyangumi usiku na mchana sikutatu Matayo 12:40 pia luka 11:30 Maana kaa vile yona alivyo kuwa ishara kwa waumini, ndivyo itakavyo kuwa kwa mwana wa Adam kwa kizazi hiki.

Mashaidi wote wawili wana sema alisema hivyo. Yona 2:1-10 Ndipo yona akamwomba bwana katika tumbo la samaki. (1) maiti hawezi kuomba YONA 2:7 roho yangu ilipozima ndani yangu maana Yesu aliziia tu.

YONA 2:10- Bwana akasema na yule samaki nae akamtapika

Je ikiwa Yesu akapona pote palipo muhusu Yona je Kurani ikisema hawa kunua ndio anakuwa sio Yesu? Je ikiwa Yesu alipona palipo muhusui yona je Kurani ikisema hawa kumuua ndio anakuwa sio Yesu?

Hoja ya hawakumsulubu

Yohana 19:33-34 lakini walipomjia Yesu na kuona yakuwa ametestiwa kufa hawakumvunja mifupa .hapa sababu ambayo ni fupi hawa kuitoa kwa sababu walimuona amaeisha kufa hawa kumvunja mifupa . Tendo lakufa ilikuwa ndio msemo wa YONA 2:7 ROHO YANGU ilipo zimia

Je kwanini hawakumvunja ?

YOHANA 19:36; Kwa maana hayo yalitokea ili andiko litimie hapana mfupa wako utakao vunjwa.

Je andiko hilo lipo wapi na linasemaje ?

ZABURI 34:19-21

Mateso Yesu aliyoyapata maana maandiko yanasema mateso ya mwenye haki ni mengi lakini Bwana humponya nayoyote. Je Yesu alikuwa hana haki?

20. Huifadhi mifupa yake yote haikuvunjika hata mmoja

21. Uovu utamua asiye haki.?

Yani wale wezi wawili sio Yesu maana yeye alikuwa mwenye haki Hivyo haiwezekani miguu sivunjwe ilikutimiza ndiko halafu asitimize na andiko la uovu kumua asiye na haki Hivyo bila shaka Yesu ndie Issa mwana wa Mariyam mwa na wa Yesu alikuwa ameisha soma maandiko hayo yanasema wazi Yesu hawakumua sababu wao walimuona tu ametulia wakasema ameisha kufa . Hivyo kurani kusema hawakuwa na yakini nalo sio kosa maana macho sio kipimo

Ikisema mifupa ilipona imekosea wapi?

Ndio kusema muda huo ilipo kuwa Qurani ikitoa hukumu tayari watu walkuwa wameisha kuwa na Imani ya kusafisha uovu wao kwa damu ya mwenzao .

Sasa wakisikia Qurani inawaambia yule mtu walioe muamini kuwa amekufa kwa ajili yao hakufa kwanini wasipinge?

Lakini hata wakipinga wasiseme Issa sio Yesu maana wanathielogia wengi dunia wanakubali ISSA NDIE Yesu.

Mwenye masikio na Asikie

Mwisho

MAKHZAN e TASAWEER
IMAGE LIBRARY

Tangazo muhimu kuhusu picha za Masihi Aliyeahidiwa (as) na Khulafa-e Ahmadiyyat

Picha za kihistoria za Jamaat, haswa zile za Masihi Aliyeahidiwa (as) na Makhalifa wake, zilipigwa na teknolojia na vifaa vya wakati wao.

Kwa masikitiko, sasa tunaona kwamba wanajamaat wengine wanazihariri na kwa kweli wanazibadilisha picha za Masihi Aliyeahidiwa (as) kupitia teknolojia ya kisasa na kuzipakia kwenye mitandao ya kijamii.

Tafadhali kumbuka kuwa majaribio ya kuhariri/kughushi picha kama hizo za thamani sio sawa na husababisha masuala anuwai.

Hivi karibuni picha ya Masihi Aliyeahidiwa (as) ilichapishwa kwenye mtandao wa kijamii na kuenea haraka kotekote. Picha hii ilitolewa kutoka picha ya pamoja na kisha kuhaririwa.

Matokeo yake ni kwamba sehemu ya ndevu za Masihi Aliyeahidiwa (as) ilikuwa ina uwaa, wakati sehemu nyingine haikuwa nayo na haikustahikiana na uso uliobarikiwa wa Masihi Aliyeahidiwa (as). Tafadhali jiepushe na mazoea kama haya yasiyofaa na mabaya.

Kwa kuzingatia haya hapo juu, wanajamaat wameagizwa kutumia tu picha zilizoidhinishwa za Masihi Aliyeahidiwa (as) na Makhalifa wake na hazipaswi kubadilishwa au kughushiwa kwa njia yoyote.

Makhzan-e-Tasaweer, London

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

DH.HIJ-MUHARR.1443 AH | AGOSTI 2021 | ZAHOOR 1400 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu^{saw}

Mjumbe wa Allah^{saw}. amesema: Yule anayejenga msikiti kwa ajili ya Allah, Allah Atamjengea (nyumba) mfano wake katika Pepo. (Muslim).

Baraka za Jalsa Zilizoshuhudiwa Ulimwenguni Kote

Katika hotuba ya Ijumaa iliyotolewa katika Jalsa Salana ya Uingereza tarehe 13/08/2021; Baada ya Tashahhud, Ta'awwudh na Surat Faatihah, Khalifa Mtukufu V, Hazrat Amir ul Momeniin, Mirza Masroor Ahmad^{atba} ('Ayyadahullahu Ta'ala Bi-Nasrihil Aziiz') alisema Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba Jalsa Salana UK imefanyika baaada ya miaka miwili. Mwaka 2020 Jalsa haikufanyika kwa sababu ya Korona.

Wasimamizi wa Jalsa Salana wakawa wanadhani kwamba Jalsa Salana haitafanyika mwaka huu pia. Kwa hiyo wakati walipoambiwa wafanye maandalizi ya Jalsa Salana walikuwa hawafanyi matayarisho vile ilivyotakiwa. Lakini walipokumbushwa kwa msisitizo kiasi fulani wakachangamka mara moja. Lakini Wafanyakazi wetu wa kujitolea wanaofanya shughuli zote wakaonekana kana kwamba walikuwa tayari hapo kabla.

Kwa kuwa Jalsa haikuwa kubwa kama kawaida yake kwa sababu ya mlipuko wa Korona, wafanyakazi wa kujitolea wakachaguliwa wachache. Lajna wakachagua sehemu ya tano ya wafanyakazi wa kawaida yao ya zamani na wanaume wakachagua sehemu ya tatu. Wale wasiochaguliwa wakumbuke kuwa Mwenyezi Mungu Hutoa ujira sawa na nia na malengo ya watumishi wake, kwa hiyo ni mategemeo yetu kwamba nyinyi pia hamtakosa thawabu yenu.



Hadhrat Khalifatul Masih V^{atba} akitoa hotuba ya Ijumaa katika Mkutano wa Mwaka (Jalsa Salana) wa Uingereza 2021

Khalifa Mtukufu (atba) alisema; ninawashukuru wahudumu wote, ambao walifanya kazi kwa nguvu zao zote, hasa katika kutoa magari maegeshoni kana kwamba walibeba magari wenyewe kutoka maegesho yaliyojaa matope. Watu wetu na wale wasiokuwa Waahmadiya walishangazwa sana na mandhari hayo yote. Hawa ndio watu wanaofanya kazi zao kama majini.

Vivyo hivyo wageni waliohudhuria Jalsa Salana na wengine walioona Jalsa Salana kupita idhaa ya MTA wameathirika na kupendezwa sana na mandhari ya shauku, na huduma za watu wenye kupika vyakula, na wenye kutengeneza mahema, na wenye kazi mbalimbali.

Khalifa Mtukufu (atba) alisema; MTA imerusha duniani kote Jalsa Salana kwa njia hii kwamba watu wameshangazwa na huduma zao. Nawashukuru wafanyakazi wote wanawake na wanaume kwamba katika hali na msimu mgumu wao wametimiza haki za kujitolea kulikoleta ufaulu wa Jalsa Salana.

Khalifa Mtukufu (atba) alisema: Zile sifa na shukrani nilizozipokea na naendelea kuzipokea kutoka dunia nzima zimenifanya niongee kuhusu maoni yao katika hotuba yote ya leo.

Khalifa Mtukufu (atba) alisema; watu wameniuliza jambo moja tu kwamba walikuwa na hamu sana ya kuona kufanyika kwa Baiat ya kimataifa. Lakini kwa sababu ya tahadhari ya kuenea kwa korona haikuweza kufanyika.

Mwaka huu jumuiya mbalimbali za nje ya UK zilishiriki kwa njia ya mitandao na idhaa ya MTA katika kushiriki na kuona Jalsa Salana UK. Miongoni mwao ni Wanajumuiya wa Australia, Guatemala, Indonesia, Tanzania, India, Uholanzi, Ufransa, Finland,

Endelea uk 4

KITABU KIPYA



Majibu ya Maswali Manne ya Mkristo Sirajuddin

Hii ni tafsiri ya Kiswahili ya *Siraj-ud-Din 'Isaa'ee Ke Chaar Sawaalon Kaa Jawaab-**Majibu ya Maswali Manne ya Mkristo Siraj-ud-Din*** yaliyoandikwa na Masihi Aliyeahidiwa na Mahdi, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, amani iwe juu yake. Kitabu kinaangazia imani zifuatazo katika kujibu maswali ya Mkristo:

- Mafundisho ya Kikristo ya uokovu kupitia inayoitwa kafara ya mlaaniwa ni chukizo na kumkufuru Nabii mpendwa wa Mungu.
- Yesu, amani iwe juu yake, hakufa msalabani na hakulaaniwa kamwe.
- Quran Tukufu imeikamilisha dhana ya Tauhidi (Umoja wa Mwenyezi Mungu), ingawa pia ilikuwa kanuni ya kimsingi katika vitabu vilivyotangulia.
- Mafundisho ya kiulimwengu ya Qur'ani Tukufu ni kwa watu wote na nyakati zote, wakati vitabu vya awali viliyawekea mpaka mafunzo yao kwa watu maalum kwa nyakati maalum.
- Uislamu unaamuru upendo kwa Mungu tu, wakati kwa uhusiano na wanadamu unafundisha rehema na huruma.
- Vita vilivyopiganwa na Mtukufu Mtume Muhammad, amani na baraka za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, vilikuwa vya kujihami kiasili na havikukusudiwa kuulazimisha Uislamu juu ya wengine.

Haya ni baadhi ya mafundisho ya hali ya juu ambayo yaliyoiasisi Ahmadiyyat katika harakati za ubashiri wa Kiislamu duniani ilivyo leo.

Jipatie nakala yako kwa bei ya maktaba ya Tsh· 3,000/=

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com